wako bibi

Je akina dada wengi hugeuka wizi ?

"Kweli dunia imekwisha kubadilika, wasema wazee ! Tunapigwa na mshangao mkubwa wakati tunaposikia ao kujionea wenyewe mambo ya aibu yanayotendeka siku hizi hapa mjini Bukavu.

Hapa zamani, mababu zetu walitia matumaini makubwa juu ya wabinti wao. Kwa kuwa kazi ya kuadibisha na kuwalea watoto ilikuwa ikimuelekea mama, iliombwa kwa akina dada kuwa na mwenendo mwema. Ndio maana wabinti walikuwa wakichunguzwa sana.

Matumaini hayo kwa watoto wanawake ilionekana tena wakati wakoloni walipofika barani Afrika. Wazungu walipendelea sana kuwakabizi wabinti kati ya kulinda feza

kwani walikuwa mbali ya pupa kali ya feza na hawana mashawishi ya kuzichopoa.

Kwa siku za leo, wamama wengi wamekwisha kupoteza ubora na zamiri njema tulioachiwa na mababu zetu. Wamoja kati ya akina mama wajiruhusu hata kuingia katika magari ya uchukuzi na kutafuta kutoka ndani bila kulipa.

Huko sokoni, kwapitika mambo ya haya. Wajiruhusu kulipisha wanunuzi biashara walivyokwisha kununua. Na wengine wasema kuwa feza walizopewa hazienei !

Ukichungua daftari ya wamama wanaofungwa jelani utatambua kupokonya feza za mashirika wanayotumikia ao za serikali.

Sisi wote tunaelewa fumbo la hayati Lumumba alisema : "Ukiadibisha mama, unaadibisha taifa lote". Na leo baba Mobutu hutia kinamama fasi inayoonekena. Wakati wamama hao wanapojiingiza katika mambo ya wizi, watoto wao watafuata mfano wa nani ?

Mwanamke anaponaswa katika mambo ya wizi anapoteza heshima aliyokuwa nayo katika jamaa na hata mbele ya majirani. Angalisho mama wapenzi, tuache wizi. Tusitumie hasa vikwembe vyetu kwa kufichikamo vitu vya wizi !

Alamsiki.
Bujiriri Mwangaza.

JE UMESIKIA ... ?

KWAMBA kutafuta mali na kinguvu kwatusukum tuonekane kama wevi ? Siku hizi, jambo hilo lajionyesha katika shirikisho llinalojidai kuwa na shuruli la kusaidia na kuamua magonvi kati ya wafanyabyashara wa Bukavu na wale wa kandokando (M.E.A.)
Kisha kunyonya feza za wanamemba wao ambazo wazikongoa kila mwezi, prezidenti wa kiungo hicho pamoja na rafiki zake wasikilizana kwa kuzitumia katika uchumi wao na zingine katika machupa ya Simba na Tembo kwani siku hizi wameachana na Kasigisi pamoja na Primus.
Akina dada mmoja ambaye alikuwa hapo hawali mlinda feza wa kiungo hicho, aliamua kujiuzulu (démissionner) ?

KUWA kunywa pombe bila kiasi kwapoteza mawazo? Kisha kumeza vilauri kazaa vya mvinyo na kanyanga kiongozi wa masomo ya msingi, Bingwa ya pale Bagira aliamua amlete mama mmoja kahaba katika biro yake na kuanza kulala naye kubaya. Bahati yake mbaya alinaswa kinyoka-nyoka na mwanafunzi wake ambaye alitumwa na mwalimu aje kutafuta chaki. Punde kidogo, alitaka tena kushika kinguvu, mwanafunzi Bora wa somo la sita. Huyo akalalamika mpaka wazazi wake wakaja kumuonyesha kiongozi huyo cha mtema kuni. Ni alama wazi ya ukosefu wa zamiri njema ya kazi. Viongozi wa masomo ya msinji wa sekondari, mwasema-je mbele ya jambo hilo ?

Tuzungumuze

Adabu ya saa zote kwa madereva

Tulipokea ofisini mwetu maandishi ya mwananchi Kimengele Kimode, msomaji wetu wa pekee, kuhusu namna ambayo twaombwa kutenda nafasi tunakoishi. Katika mistari ifuatayo, twachapa maelezo inayoelekea madereva katika kazi wanayoifanya.

Hapa nitasimulia juu ya yule ambae gari si lake, yule ambae kutembeza gari ndio kazi yake. Maana yake yule anayetumikia mtu mwengine au chama fulani.

Ukiwa dereva jua kama gari si lako na kama bila gari lile utabaki "mlofwa". Ndio maana daraka zako ni za aina mbili.

Kwanza : Kwa kuwa gari si lako upo mtumishi tu na si mwenyeji. Kumbe azimio la utimizi wa gari halitatoka kwako wewe balikwa mwenyeji. Kazi yako wewe ni kuongoza gari na kulipeleka kule ambako waliliainisha, kwa mda wa kufaa na kwa kazi ikifwatana na kawaida ya mwenyeji.

Pili : Kwa kuwa gari hilo ndio shamba lako hauna budi kulitunza vema ili usikose kazi na matunda ya kazi yako yasikuepe.

Ukiwa dereva wa "voiture" au wa "auto-bus", na kadhalika onyesha kama umeadibika ukimpatia kila moja heshima yake. Watu unaowabeba garini mwako si watu wako, si watumishi wala watu chini ya uwezo wako. Sivyo. Wakiwa katika "autobus" ni sababu walilipa safari yao. Wale ambao unabeba katika "voiture" ni sababu mwenyeji wa gari alikuambia uwasafirishe. Wanaweza kuwa ndugu zake, marafiki ama wakubwa wake wa kazi au wakubwa wa Serikali. Kumbe wakati ule ni wenyewe ndio wenyi kumiliki gari, ni wenyewe ndio wenyi kukumu, ndio wenyi uwezo juu ya gari na juu yako. Uwe, kumbe, mwenyi adabu kwao:usisimame mahali bila ruhusa yao, ufwate njia yao na usifuate yako binafsi. Katika maneno na matendo yako malezi mema na mwenendo bora vionekane, vikufanye mpendekevu mbele za wageni wale.

Unaposafirisha wa akina-bibi hauna budi kuwa mvumilivu. Ujisahau mwenyewe binafsi kwani bila sadaka hiyo masikilizano ni mwiko. Pia ni daraka yako kulinda siri. Unaposafirisha wakubwa wako au wa akina-bwana wengine, hebu ulinde siri. Usivumbue siri zao kwa kuwa ulizisikia. Linda ulimi wako na usijipotezee matumaini.

Ukiwa dereva wa chama fulani (société) na kama unapashwa kusafirisha mwenzako somo wa kazi lakini mwenyi kukupita cheo (grade) umheshimie ukifwata njia ambao anakupasulia yeye. Usijiruhusu kukanata wasafiri na kuwabeba garini bila ruhusa yake, usisimame pale upendapo bali mahali akuambiapo usimame. Kwani kwa mda mnapokuwa pamoja ni yeye mnyapara wa chama na wakubwa wa chama.

Maneno yako yawe kamili na matendo yako bora. Usitamke maneno ya washarati unapobeba wakubwa wako wa kazi na unapopita penyi mgi usiwapigie wasichana yowe. Kwani mwenendo wa aina hiyo ni ishara ya maadibiko mabaya na ni dalili ya kukosewa hekima.

Kimengele Kimonde.-

JUA

Gazeti la Kivu

Kabare

Liwali Mwando : "Hatutaki fujo bali maendeleo ya mtaa wa Kabare"

Siku ya nne, tarehe 27 marsi 1985, Presidenti wa chama aliye pia liwali wa jimbo la Kivu, mwananchi Mwando Nsimba alijielekeza Lwiro, ambako aliwakusanya viongozi mbali mbali wa mtaa wa Kabare (mikoa pamoja na vijiji). Wasomaji wetu wataelewa kuwa, mheshimiwa huyo atembelea siku hizi vijiji vya asili kusudi apate kuelewa na kujionea mwenyewe namna gani viungo vya chama vyaongozwa. Bila kusahau uchunguzi wa kazi za maendeleo ambazo ni msinji wa kuimarisha maisha ya wakaaji.

Alipowahotubia viongozi wa mtaa huo wa Kabare liwali Mwando aliwaomba waungane mkono kusudi mtaa wao upate kusonga mbele. Wale wanaoleta fujo huko Kabare (kiongozi wa mtaa, washauri wake pamoja na "bajinji" waliombwa kutupilia mbali fitina wanayo na hiyo kwa mafaa ya raia wanaowaongoza.

Hapo mbele, viongozi hao walimshitaki mwami Kabare Ntayitunda wakisema kuwa yeye ndiye msinji wa kurudisha nyuma maendeleo ya mtaa wao. Wasema kuwa Kabare ni mwivu na ajiruhusu kila mara kunyanganya watu mali zao (shamba na ufu go).
Walipoulizwa na liwali Mwando, viongozi hao wa mtaa wa Kabare walikubali kuwa ni wao ndio waliweza kuandika vibarua vya kumshtaki mwami Kabare ambaye apendaka kuongoza mkoa wake mwenyewe bila asipewe mashauri na mtu mwengine.

Liwali Mwando aliwapasha kuwa mambo yote waliomwelezea ameisikia na yupo tayari kutoa ripoti kwa wakuu wake wa kazi.

Siku ya kwanza, tarehe 1 aprili ijayo, mwananchi Mwando atatembelea tena mtaa wa Kabare ambako atachungua hospitali ya Mukongola kisha kujionea kazi zinazoendeshwa na wataliana wanahusika na kulinda mbegu za kupanda (semences) huko Birava.

Katika safari yake liwali Mwando yupo mwenyi kusindikizwa na wananchi Sekimonyo na Magango na Mandoko Mabongoy, wa kwanza akiwa presidenti wa baraza la jimbo na wa munyampara wa wilaya ya Kivu ya kusini.

Padre Mulindwa katimiza miaka 19 ya kiaskofu

Siku ya Mungu tarehe 24 Marsi 1985, waumini wa dini ya kikatoliki wanaobaki jimboni mwa Kivu walisherehekea miaka 19 ya kazi ya kiaskofu ya Padre Mulindwa Mutabesha, hapo zamani Aloys. Sherehe za siku kuu hiyo, zilianzishwa na miisa mikubwa iliyosomwa na mheshimiwa huyo ambaye alikuwa akizungukwa na maaskofu Mambe wa Kindu, Kataliko wa Butembo, Pirigisha wa Kasongo na Ruhamanyi, msaidizi wa arkiaskofu nia manadri wengi kutok[illegible] pande nne za jimbo la Kivu pamoja na wafrera pia mabikira.

Liwali wa jimbo la Kivu aliwakilishwa na makamu wake, mwananchi Edjonga Bokwa, Sekimonyo wa Magango, prezidenti wa baraza la jimbo la Kivu pamoja na viongozi wengi katika chama na serikalini.

Katika hotuba yake, arkiaskofu Mulindwa aliwakumbusha waumini wote kuwa kazi za kilazima hapa duniani ni zile za kujenga kanisa moja na [illegible] kuishi mape[illegible]ndo, amani, uhaki katika ujima mkubwa (grande collaboration). Yafaa pia kuwaunga mkono wachungaji pamoja na wakuu wa serikali.

Katika masemi yake arkiaskofu Mulindwa alinena kuwa kutafunguliwa mwaka kesho seminari kuu hapo Buhimba-Goma

Kwa kumaliza sherehe hizo, akina bwana arkiaskofu Mulindwa aliwapa wahuzuriaji baada ya karamu ya heshima aliyowaandalia baraka ya mwenyezi Mungu kusudi wapate mwanga wa milele.

Bisimwa L. - B. Tserou